

UJENZI WA BANDA LA NG'OMBE:

Umuhimu wa kuwa na banda kama ifuatavyo:

- Usalama wa mifugo
- Kuepuka migongano kati ya Jamii inyomzunguka mfugaji
- Njia mojawapo ya kumtiisha
- Kumpunguzia ng'ombe adha ya jua na mvua

MAMBOYA KUZINGATIA WAKATI WA UJENZI WA BANDA

- Kuifahamu jiografia ya mahali banda litakapo jengwa.
- Mahusiano yaliyopo kati banda na mahitaji mengine ya jamii iliyo karibu
- Uwezo wa mfugaji kifedha/mtaji
- Idadi ya ng'ombe wanatarajiwa kukaa bandani
- Muelekeo wa upepo
- Upatikanaji wa maji
- Nguvu kazi itakayoshiriki katika ufugaji

SEHEMU MUHIMU ZA BANDA LA NG'OMBE:

Banda lina sehemu kuu 4 kama ifuatavyo:

- **SEHEMU YA KULALA:** Sehemu hii mara nyingi husindiliwa udongo ili kuhakikisha ng'ombe hatumii nguvu nyingi kuzalisha joto la kutosha kukabiliana na baridi. Udongo mara upatapo joto hulihifadhi kwa muda mrefu. Chumba cha kulala ng'ombe kinakuwa na upana wa sm 110 – 120 na urefu wa sm 200. Idadi ya vyumba vya kulala hutegemea idadi ya ng'ombe watakaofugwa kwa kuanzia.
- **SEHEMU YA MATEMBEZI:** Sehemu hii hujengwa imara kwakutumia zege kali ya uwiano wa 1:3:6 kwa maana ya kipimo 1 cha sementi, vipimo 3 vya mchanga na vipimo 6 vya kokoto. Vipimo maana yake chombo chochote utakachotumia kupimia uwiano huo. Mfano chepe 1 la sementi, chepe 3 za mchanga na chepe 6 za kokoto. Zege ikisha mwagwa haipigwi kibao kwa maana ya kulainisha kuepuka kuteleza kwa ng'ombe. Sehemu hii ina urefu wa sm 250 na upana unategemea idadi ya ng'ombe wanaojengwea banda na malengo ya mfugaji ya sasa na baadaye.

- **SEHEMU YA KULISHIA NA KUNYWESHEA MAJI:** sehemu hii hujengwa mbele ya sehemu matembezi na wakati mwingine huunganishwa kwa zege ya moja kwa moja na kutenganishwa na nguzo na papi zitakazo pigiliwa kumzuia ng'ombe asitoke. Aidha, wakati mwingine mfugaji hujenga sehemu hii kwa kupigilia mbaao kwa umaridadi mkubwa ama tofali kutegemea kiasi cha fedha alichonacho. Hemu hii itakuwa na upana wa sm 80 na urefu kwa kutegemea idadi ya vyumba vya ng'ombe.

Kisima cha maji huunganishwa na sehemu hii kwa kujengwa pembeni mwa upande mmojawapo wa banda na hasa ule ambao hauko karibu na kibanio au katikati. Ikumbukwe kuwa maji kwa ngombe ni muhimu na hivyo banda ambalo halina kisima cha maji linahesabika halija kamilika. Vipimo vya kisima ni urefu wa sm 80 kwa upana wa sm 60 kwa kina cha sm 50.

- **SEHEMU YA KIBANIO:** Sehemu hii ni muhimu sana kwa ajili ya kumtiisha mnyama kwa ajili kumpa huduma na kukamulia. Sehemu hii ni lazima ijengwe imara kwa vile mara nyingi siyo sehemu rafiki kwa ng'ombe. Mara nyingi sehemu hii hujengwa mahali ambapo ni rahisi kupafikia na hasa wakati wa kukamua. Kipimo cha sehemu hii ni urefu wa sm 160 na upana wa sm 100.

Imetayarishwa na

Dr.Poul Y. Kisaka (Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi)

